UMOJA WA MATAIFA
TANZANIA

# Kuzuia unyanyasaji wa kijinsia na ukatili

Ujumbe muhimu



MTANDAO WA ULINZI DHIDI YA UNYONYANJI NA UKATILI WA KINGONO TANZANIA

## Tambua

**Unyonyanji na ukatili wa kingono hauruhusiwi kabisa.**

Fahamu taratibu na shika kanuni sita za msingi kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na ukatili.

1. Kufanya unyanyasaji wa kijinsia ni sababu tosha ya kukoma kwa ajira.
2. Imekatazwa siku zote kushiriki ngono na yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18.
3. Imekatazwa kubadilishana fedha au vitu kwa fadhila ya ngono.
4. Hakuna uhusiano wa kingono unaoruhusiwa kati ya washiriki na jamii zinazoathirika.
5. Ni lazima kutoa taarifa kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na ukatili (ni lazima kwa wote!)
6. Ni wajibu wa jumla wa utawala kuzuia na kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia.

✓ PATA HABARI KUHUSU KUZUIA UNYANYASAJI NA UKATILI WA KINGONO

✗ HAKUNA MSAMAHA KWA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Fahamu na fuata sheria na taratibu na jifunze zaidi kuhusu unyonyanji na ukatili wa kingono. USIJARIBU kuchunguza kama dai ni la kweli au hapana.

## Toa taarifa

**Kutoa taariza za unyanyasaji wa kijinsia ni lazima kwa watoa huduma wote.**

- Ni sharti utoe taarifa kuhusu mambo yote yanayosababisha wasiwasi, mashaka, au uvumi kuhusu unyonyaji na ukatili wa kingono.
- Ni muhimu kufuata utaratibu wa ndani wa shirika lako wa kutoa taarifa uliowekwa na kupokea malalamiko.
- Kutoa taarifa, unaweza siku zote:
  - Kuongea na Mtoa Taarifa za unyonyaji na ukatili wa kingono katika eneo lako.
  - Kuwasiliana na Mratibu wa shirika wa Ndani wa unyonyaji na ukatili wa kingono.
  - Wapigie C-SEMA (116, namba isiyotozwa kuomba muongozo wa kufuata)

✓ TAMBUA NA TOA TAARIFA

✗ USICHUNGUZE AU KUTATUA TATIZO

Usijaribu kuchunguza kama madai ni ya kweli au la.

## Chukua hatua

**Kila mtu anapaswa kufahamu jinsi ya kuchukua hatua iwapo mhanga anahitaji huduma kutoka kwako.**

- Wakati wote fikiria usalama na ustawi wa mhanga.
- Heshimu usiri na matakwa ya mhanga.
- Toa taarifa sahihi kwa mhanga kuhusu huduma zote zinazopatikana, ikiwa ni pamoja na msaada wa matibabu na msaada wa kisaikolojia ya jamii (iwapo umeombwa na mhanga, umuelekeze).

✓ SIKILIZA NA ULIWAZE

✗ USIKOSOE AU KUHUKUMU

Usalama na heshima ya waathirika inapaswa kuwa kipaumbele cha kwanza kwa watendaji wote wa maendeleo na kibinadamu. Rufaa kwa Huduma za msaada ni muhimu na pia ni haki ya mwathirika.

**Ili kuripoti tukio:**

*Shirika:* | *Jina:* | *Barua pepe:* | *Tovuti:* | *Namba ya simu:*